JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA NANE

KIKAO CHA KUMI NA TATU

10 FEBRUARI, 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA NANE

KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 10 FEBRUARI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Posta Tanzania, kwa Mwaka 2008 *[The Annual Report and Accounts of The Tanzania Postal Bank for the Year 2008].*

The Mid-Term Review of The Monetary Policy Statement of The Bank of Tanzania for the Year 2009/2010.

MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini juu ya Taarifa ya Serikali kuhusu ubinafsishwaji wa Mgodi wa Kiwira.

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu Mchakato wa Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura ulioipa Ushindi Kampuni ya Richmond Development Company LLC ya Houston Texas – Marekani Mwaka 2006.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu uendeshaji usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania uliofanywa na Kampuni ya ***RITES*** ya India.

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu Utendaji wa kazi usioridhisha wa Kampuni ya ***TICTS.***

II. MASWALI:

WAZIRI MKUU:

145. MHESHIMIWA HERBERT JAMES MNTANGI (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kwa kuwa, kiasi cha fedha kinachopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Jiji ni kikubwa na kinahitaji usimamizi wa ziada; na kwa kuwa, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kipo chini ya Mkurugenzi Mtendaji:-

Je, mfumo wa kulazimisha taarifa ya Ukaguzi wa Ndani ipitie kwa Mkurugenzi Mtendaji kabla ya kupelekwa kwenye Kamati ya Fedha haufanyi Mkaguzi wa Ndani kukosa uhuru wa kutoa taarifa sahihi.

146. MHESHIMIWA DK. LUKA JELAS SIYAME (MBOZI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kwa kuwa, Mji Mdogo wa Tunduma unakua haraka kiasi cha kuathiri mwenendo wa Utawala Bora na utoaji wa Huduma za Jamii:-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi ya Mji huo kuwa Mji kamili ili uwe Halmashauri na hivyo kuwa na Jimbo la Uchaguzi linalojitegemea.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:

147. MHESHIMIWA MWAKA ABRAHMAN RAMADHAN (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Kwa kuwa, Tanzania ina chombo kimoja cha kukusanya kodi yaani Mamlaka ya Mapato Tanzania **(TRA):-**

Je, kwa nini gharama za ushuru wa magari yanayoingizwa katika mpaka wa Holili - Moshi zinatofautiana na gharama za Bandari ya Dar es Salaam.

148.MHESHIMIWA RIZIKI OMAR JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Kwa kuwa, tarehe 5/02/2009 Shirika la Bima **(NIC)** lilitangaza kusitisha huduma kwa muda wa siku mbili ambapo wafanyakazi wapatao mia tano (500) walisimamishwa kazi na wakaajiriwa wengine:-

(a) Je, mchakato wa uajiri ulitegemea vigezo gani na je, muda wa uajiri ulitosha;

(b) Je, kuna vyombo vya habari vilivyotumika kutangaza ajira hizo mpya.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

149.MHESHIMIWA PROF. RAPHAEL BENEDICT MWALYOSI (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kwa kuwa, ni Sera ya Serikali kuboresha kilimo cha umwagiliaji na wakati huo huo kuna Sera ya kuhifadhi vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na maeneo oevu:-

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kuwa sera hizo mbili hazigongani;

(b) Je, Serikali itahakikishaje kuwa miradi ya umwagiliaji inakuwa endelevu.

150. MHESHIMIWA JACOB DALALI SHIBILITI (MISUNGWI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kwa kuwa, Serikali ilitenga Bilioni 1.2 kwa ajili ya Mradi wa Maji Mjini Misungwi kwa dharura; na kwa kuwa, iliahidi kwamba muda mfupi maji yangepatikana:-

(a) Je, ni hatua zipi za utekelezaji kwa sasa zimefikiwa;

(b) Je, ni tatizo gani limefanya kucheleweshe Mradi huo wa dharura.

WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

151. MHESHIMIWA JOHN PAUL LWANJI (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Kwa kuwa, Shirika la Posta Mjini Itigi linatoa huduma kwa kutumia jengo la kukodisha la Shirika la Reli Tanzania **(TRL);** na kwa kuwa, jengo hilo ni dogo na chakavu:-

Je, ni lini Shirika la Posta litajenga Ofisi kubwa Mjini Itigi yenye kulingana na hadhi ya Mji huo wenye watu wengi.

152. MHESHIMIWA DKT. BINILITH SATANO MAHENGE (MAKETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Kwa kuwa, moja ya sababu zinazosababisha nchi za Afrika kuendelea kuwa masikini ni kuwa nyuma katika maendeleo ya Sayansi na Teknolojia; na kwa kuwa, Sera ya Sayansi na Teknolojia ya Mwaka 1996 inaelekeza kuwa, masuala ya Sayansi na Teknolojia, yaingizwe kwenye Mpango wa Taifa wa Uchumi (National Economic Plan) kwa kuanzisha mfumo wa kushirikisha Wanasayansi na Teknolojia katika

maandalizi ya Mpango wa Maendeleo ya Uchumi wa Taifa:-

(a) Je, ni Wanasayansi na Wanateknolojia wangapi walio katika Tume ya Mipango ya Taifa;

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuandaa wataalam watakaosimamia mali za asili kama gesi, mafuta nk. zilizogunduliwa nchini.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:

153. MHESHIMIWA MARTHA JACHI UMBULLA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko:- Kwa kuwa, ishara ya kukua kwa uchumi wa nchi ni ukuaji wa Sekta ya Viwanda na Biashara, na siyo kutegemea kilimo kama ilivyo hapa nchini; na kwa kuwa, hivi sasa Serikali inahimiza sana uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa ajili ya chakula na biashara:-

Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kuwa uzalishaji wa mazao ya kilimo unaenda sanjari na kuanzisha Viwanda Vidogo na Masoko ya uhakika ili kukuza uchumi wetu.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

154. MHESHIMIWA EMMANUEL JUMANNE LUHAHULA (BUKOMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kwa kuwa, Ilani ya **CCM** ya mwaka 2005; Ibara ya 111(a) inaeleza kuwa na Majeshi ya Ulinzi wa Wananchi na Usalama wa Raia; na kwa kuwa, katika Msitu wa Ushirombo – Runzewe ujambazi na utekaji wa magari umekuwa tishio kwa wananchi wa Bukombe:-

(a) Je, Serikali inapata faida gani kwa wananchi wa Bukombe ambao wanapoteza maisha na mali zao kwa sababu ya ujambazi huo; kama hakuna faida; Je, Serikali inaona ugumu gani kupeleka **JWTZ** kulinda maeneo hayo;

(b) Je, kwa nini Serikali isiugawe msitu wa upande mmoja kwa wafugaji kama njia ya kutekeleza Ilani ya **CCM**; kwa maana ya ulinzi na kutenga maeneo ya malisho kwa wafugaji.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

155. MHESHIMIWA SIRAJU JUMA KABOYONGA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Kwa kuwa, Mkoa wa Tabora kihistoria ni maarufu kwa shule mashuhuri hapa nchini ambazo Watanzania wengi mashuhuri wamesoma, kwa mfano Shule za Sekondari za Tabora Wavulana na Wasichana pamoja na Milambo (St Marys') ni za miaka mingi lakini shule hizo zinazidi kupoteza umaarufu wake kadiri miaka inavyoendelea; na kwa kuwa, uanzishwaji wa vyuo vikuu hapa nchini umeshamiri lakini mpaka sasa hakuna Chuo Kikuu kilichoanzishwa Tabora Mjini zaidi ya Chuo Kikuu Huria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Chuo Kikuu Mjini Tabora kwa lengo la kuendeleza historia ya elimu kwenye Mkoa huo kama kitovu cha elimu hapa Tanzania.

156. MHESHIMIWA MGENI JADI KADIKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Kwa kuwa, Serikali imehamasisha wanafunzi wa kike wasome ili baadae washike nafasi mbalimbali za utendaji maofisini kuendana na dhana ya kuwa na uwakilishi asilimia 50 kwa 50 (50/50); na kwa kuwa, kuna udhaifu mkubwa kwa wanafunzi wa kike mashuleni

kupata mimba kwa wingi hasa wale wanaojiweza kimasomo:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa, mimba zinapungua mashuleni ili kuendana na lengo la 50/50.

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

157. MHESHIMIWA JOB YUSTINO NDUGAI (KONGWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Kwa kuwa, malaria ni ugonjwa hatari unaosababisha vifo vingi hapa nchini; na kwa kuwa, Serikali imedhamiria kuangamiza mbu wanaosababisha malaria kwa kutumia kemikali ya **DDT**:-

(a) Je, Serikali inawahakikishiaje Watanzania juu ya usalama wa maisha yao, mimea, wanyama na viumbe wengine;

(b) Je, hakuna kemikali nyingine zinazoweza kutumika ili kuepuka kutumia **DDT** hapa nchini.

WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

158. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Kwa kuwa, kwa muda mrefu kumekuwepo na kilio cha njaa sehemu nyingi nchini; na kwamba Serikali bado haijfikia lengo la kuitumia mito isiyokauka na mabonde yenye rutuba kuleta mapinduzi ya kweli ya kilimo:-

Je, Serikali inajifunza nini kutokana na tatizo hili linalojitokeza kila mwaka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani.

159. MHESHIMIWA MARIA IBESHI HEWA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Kwa kuwa, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu, lakini kinategemea jembe la mkono na kwa kiasi kidogo jembe la kukokotwa na wanyama; na kwa kuwa, ili kilimo kiendelee kunahitajika kuwepo pembejeo na zana za kisasa:-

Je, Serikali ina mikakati ipi kuhusu matumizi ya zana hizo kwa wananchi wake ili kuonyesha tofauti ya tulipotoka, tulipo na tunapoelekea.

III. KAULI ZA MAWAZIRI:

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI.

IV. UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE TAASISI MBALIMBALI ZA ELIMU YA JUU:

(i) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam – Wajumbe 2;

(ii) Chuo Kikuu cha Biashara na Stadi – Mjumbe 1;

(iii) Tanzania Commission for Universities – Mjumbe 1;

(iv) Mwalimu Nyerere Memorial College – Mjumbe 1.

V. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini juu ya Taarifa ya Serikali kuhusu ubinafsishwaji wa Mgodi wa Kiwira.

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu Mchakato wa Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura ulioipa Ushindi Kampuni ya Richmond Development Company LLC ya Houston Texas – Marekani Mwaka 2006.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu uendeshaji usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania uliofanywa na Kampuni ya ***RITES*** ya India.

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu Utendaji wa kazi usioridhisha wa Kampuni ya ***TICTS.***

DODOMA
10 FEBRUARI, 2010

DKT. T.D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE